# CHUO CHA UONGOZI WA MAHAKAMA LUSHOTO
# IJA

## MAFUNZO YA MADALALI NA WASAMBAZA NYARAKA ZA MAHAKAMA

1. Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto kinapenda kuutangazia umma kwamba kinatarajia kufanya mafunzo yanayowalenga wale wote wenye nia ya kuomba na kufanya kazi ya Udalali wa Mahakama na Usambaza Nyaraka za Mahakama kwa mujibu wa Kanuni za Madalali wa Mahakama na Wasambaza Nyaraka za Mahakama, Tangazo la Serikali Namba 363 la 2017 (The Court Brokers and Process Servers (Appointment, Remuneration and Disciplinary) Rules, GN. 363 of 2017).
2. **Muda na Mahali**: Mafunzo hayo yatafanyika kuanzia tarehe **29 SEPTEMBA 2025** mpaka tarehe **13 OKTOBA 2025** katika Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo Tanzania (Law School of Tanzania) jijini Dar es Salaam.
4. **Sifa za Washiriki**: Muombaji anapaswa kuwa na sifa zifuatazo:-
   - Awe raia na Mkazi wa Tanzania mwenye umri wa utu uzima.
   - Awe na Elimu ya kidato cha Nne na kuendelea na awe na uwezo wa kuandika na kuzungumza Kingereza na Kiswahili kwa ufasaha.
   - Awe ni mtu mwenye tabia njema na muadilifu wa kiwango cha hali ya juu na ambaye hajawahi kutiwa hatiani kwa makosa ya jinai/yahusuyo kukosa uaminifu au uadilifu.
5. **Muombaji Asiwe:** Jaji au Hakimu aliye kazini, au mwajiriwa wa nafasi yoyote katika mahakama ya Tanzania, au Wakili wa Kujitegemea.
6. **Ada ya ushiriki**: Kwa washiriki wa mafunzo ya Udalali wa Mahakama ni **Shilingi 1,025,000/= pamoja na *kitini cha kufundishia.***
7. **Ada ya Ushiriki:** Kwa washiriki wa mafunzo ya Wasambaza Nyaraka za Mahakama ni Shilingi **695,000/= pamoja na kitini cha kufundishia.**
8. **Jinsi ya kutuma maombi:** Waombaji wanaweza kuingia katika tovuti ya Chuo www.ija.ac.tz ili kupata fomu ya maombi kisha kuijaza na kuiwasilisha chuoni kwa njia ya posta (E.M.S) au kwa anuani ya barua pepe courtbrokers@ija.ac.tz ama kufika chuoni na kuiwasilisha kwenye ofisi ya Mkuu wa Chuo.
9. Fomu ya maombi iambatishwe na:-
   - Kivuli cha Cheti cha Elimu ya Kidato cha Nne.
   - Kivuli cha Cheti cha kuzaliwa au kitambulisho cha uraia.
   - Nakala ya risiti ya malipo ya ada ya maombi ya **Shilingi 30,000**
10. Malipo ya maombi yafanyike kupitia ***namba ya malipo (Control number)***: **995700038201** mlipwaji ni **Chuo Cha Uongozi wa Mahakama Lushoto**.
11. Malipo yafanyike kupitia:-
    - Benki au Wakala wa benki ya NMB, CRDB na TPB. Tumia namba maalumu ya malipo kwa rejea ya malipo husika.
    - Mitandao ya Simu: -
      1. Ingiza namba maalumu ya muamala ya mitandao husika
      2. Chagua namba 4 kufanya malipo
      3. Chagua namba 5 malipo ya Serikali

    Tumia namba maalumu ya malipo kwa rejea ya malipo husika.
12. Kwa maelezo zaidi tembelea tovuti ya Chuo www.ija.ac.tz au piga simu namba:-**+255-27-2660133 au 0784155523, 0782-145560, 0762654075**
13. Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe **15 SEPTEMBA 2025.**

Imetolewa na:

**Mkuu wa Chuo,**
**Chuo Cha Uongozi wa Mahakama Lushoto**
**S.L.P 20**
**Lushoto**